

HOTUBA YA MHE. MAMA SALMA KIKWETE AKIZINDUA MAJENGO
MAPYA MATATU YA MADARASA, OFISI MBILI ZA WALIMU,
MSAADA WA MADAWATI NA UKARABATI WA MAJENGO YA
ZAMANI KATIKA SHULE YA MSINGI UHASHI, WILAYANI BUNDA,
MKOA WA MARA
TAREHE 18 MEI, 2011.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu,
na Mbunge Jimbo la Bunda, Bw. Steven Wasira

Mhe. Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Bw. Makongoro Nyerere

Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Bw. Isaack Mtinga

Katibu wa CCM Mkoa, Bw. N.M. Ndekubali

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Mara, Bi. Nancy Msafiri Sesani

Mkurugenzi Mkuu wa Tanzania Potland Cement Company Limited,

Ndugu Pascal Lesoinne,

Msambazaji wa Saruji ya Tanzania Potland Cement Company Limited

Kanda ya Ziwa, Ndugu Zulfikar Nanji.

Wabunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mara

Waheshimiwa Madiwani

Viongozi wote wa Chama na Serikali,

Walimu na wanafunzi,

Mabibi na Mabwana,

Habari za leo!

Napenda kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rema kwa kutuwezesha kukusanyika pamoja wakati huu hapa Shule ya Msingi Ushashi.

Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana

Leo hii ni siku ya pili ya ziara yangu ndani ya Mkoa wa Mara. Napenda kuwataarifu kuwa nimefurahishwa sana na uhisani unaotambulika rasmi leo kwa tukio hili kwani pia ndio ulionipa kupata fursa hii ya kuwatembelea wanajumuia wote – walimu,

wanafunzi, wafanyakazi mkiwemo pia na majirani wa Shule ya Msingi Ushashi, na wakazi wa Mkoa wa Mara kwa Ujumla.

Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana

Leo sitakuwa na maneno mengi. Jukumu langu ni la kutoa shukrani kwa uhisani mkubwa tuliopatiwa na ***Tanzania Potland Cement Company Limited*** ambao leo wanatukabidhi rasmi majengo matatu ya madarasa, ofisi mbili za walimu, madawati na majengo yalikaarabatiwa. Ni kazi kubwa iliyowagharimu wenzetu hawa wanaotupenda kiasi hiki takriban Shilingi milioni tisini za Kitanzania (Tsh. 90m/-).

Shukrani za pekee kabisa ziende kwa ***Mkurugenzi Mkuu wa Tanzania Potland Cement Company Limited***. Nasema kwa dhati kabisa, ASANTENI SANA kwa mchango wenu!

Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana

Umuhimu wa Kampuni hii nadhani unaeleweka. Tunaamua kujenga nyumba bora, au la majengo mengine ya kufanyia kazi za kibiashara

na huduma tunahitaji kutumia saruji iliyo bora. Na Tanzania **Potland Cement Company Limited** ni miongoni mwa makampuni yaliyo na mchango mkubwa nchini Tanzania katika uzalishaji wa saruji na ustawi wa sekta ya ujenzi kwa ujumla. Kwa kifupi ni wadau-wenza katika kuboresha makazi yetu, ofisi zetu na miundo mbinu kadha wa kadha katika sekta za ujenzi na makazi.

Ndugu Viongozi, wanafunzi, Mabibi na Mabwana

Napenda kulisema hili kama neno langu la shukrani kwao, kwamba hawakuishia tu kuangalia namna ya kuyafikia malengo yao ya kibiashara kwa manufaa ya wanahisa wao. Wametambua na kuguswa na jukumu lao la kuisaidia jamii katika kutatua matatizo hususan katika sekta ya huduma ya jamii.

Ndio maana waliamua kutumia takriban shilingi milioni tisini, kwa ajili ya kuboresha majengo na ununuzi wa madawati yanayohitajika hapa Shule ya Msingi Ushashi, Bunda.

Ninawapongeza tena na kuomba makampuni na wafanyabiashara wengine waige mfano wenu, **Tanzania Potland Cement Company Limited!**

Ndugu Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana

Ili tuweze kushinda vita ya kupambana na adui ujinga, hatuna budi kuwa na silaha muhimu zinazohitajika. Silaha hizo zinajumuisha uwepo wa walimu, zana za kujifunzia na kufundishia, ikiwemo pia miundombinu bora ya kutolea elimu. Miundombinu hii inajumuisha madarasa, ofisi za walimu, madawati na vyoo. Kwa pamoja hivi huiwezesha shule kuwa na mazingira rafiki na yenye usalama wa kiafya kwa wanajumuia wake wa ndani na wale wanaoizunguka.

Hivyo, naomba nichukue fursa hii kuwatambua na kuwapongeza viongozi na wadau wote mlioshirikiana na **Tanzania Potland Cement Company Limited**, hadi mkafanikiwa kuleta mazingira rafiki ya kujifunza na kufundisha katika shule hii.

Ni matumaini yangu pia kwetu sisi tunaoupokea msaada tunaoupokea kwa shukrani. Na tutauthamini kwa vitendo kwa namna tutakavyoyathamini na kuyatunza majengo haya, ofisi na madawati tunayokabidhiwa leo rasmi hapa Shule ya Msingi Ushashi, Bunda Mkoa wa Mara.

Ndugu Wageni waalikwa, wanafunzi, Mabibi na Mabwana

**NAPENDA NIMALIZIE KWA KUTAMKA RASMI KUWA MAJENGO (3)
MAPYA YA MADARASA NA YALIYOKARABATIWA, OFISI (2) ZA
WALIMU NA MADAWATI, YAMEPOKELEWA NA KUZINDULIWA
RASMI KWA MATUMIZI YAKE.**

Naomba niwaage kwa kuwatakieni kila la heri katika shughuli zenu
za ujenzi wa taifa!

Ahsanteni kwa kunisikiliza!